

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA KWA UMMA

TANGAZO KWA WAFANYABIASHARA WA CHAKULA, DAWA, VIPODOZI NA VIFAA TIBA KUHUSU KUHUISHA VIBALI VYA KUENDESHA BIASHARA ZA CHAKULA, DAWA, VIPODOZI NA VIFAA TIBA

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) inapenda kuwakumbusha wafanyabishara wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kuwa mwisho wa kuhuisha (renewal) vibali vya biashara hizo kwa mwaka wa fedha 2011/12 utakuwa tarehe 31/07/2011.

Malipo ya kuhuisha vibali yatakayofanyika kuanzia tarehe 1/08/2011 yatapokelewa na faini ya asilimia ishirini na tano (25%) ya gharama ya kuhuisha kibali husika.

Pia, Mamlaka ya Chakula na Dawa inapenda kuwataarifu kuwa mwisho wa kupokea malipo hayo ya kuhuisha vibali kwa mwaka wa fedha 2011/12 ni tarehe 30/09/2011. Baada ya tarehe hiyo, Mamlaka haitapokea malipo ya kuhuisha vibali na wafanyabiashara wa dawa, vipodozi na vifaa tiba ambao watakuwa hawajahuisha vibali vyao watachukuliwa hatua za kisheria.

Biashara zinazolengwa ni kama ifuatavyo;

1. Famasi za jumla zinazojihusisha na uingizaji wa dawa nchini,
2. Famasi za rejareja
3. Maduka ya vifaa tiba,
4. Maghala ya kuhifadhia chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba,
5. Maduka yote ya dawa muhimu,
6. Maduka ya chakula na vipodozi ya jumla na rejareja,
7. Viwanda vya chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba,
8. Machinjio (Abattoir and slaughter houses),
9. Supermarkets,
10. Maduka ya kuuzia nyama (butcher),
11. Migahawa, baa na kantini,
12. Mashine za kusaga,
13. Magari ya kusafirisha chakula na dawa,
14. Watoa huduma za vyakula kwenye sherehe,
15. Hoteli za kitalii na za kawaida.

Fomu za maombi ya kuhuisha vibali zinapatikana katika ofisi zifuatazo:

1. TFDA-Makao Makuu Mabibo External, Dar Es Salaam.
2. TFDA Kanda ya Ziwa- Mwanza, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini-Mbeya na Kanda ya Kaskazini-Arusha.
3. Ofisi za Waganga Wakuu wa Mikoa yote;
4. Ofisi za Waganga Wakuu wa Halmashauri za Jiji, Manispaa, Wilaya na Miji yote

Fomu hizi pia zinapatikana kupitia tovuti ya TFDA www.tfda.or.tz

Tangazo hili limetolewa na:

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA),
Barabara ya Mandela, Mabibo-External,
S.L.P 77150,
Dar Es Salaam.**

Simu: +255 22 2450512/2450751/2452108

Nukushi: 255 22 2450793

Barua pepe: info@tfda.or.tz

Tovuti: www.tfda.or.tz